



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

*Barua zote zianikwe na kutumwa kwa:*

Tel: +255 262 965732 (Direct line)  
+255 659 566703

e-mail: [ded@sikongedc.go.tz](mailto:ded@sikongedc.go.tz)

Tovuti: [sikongedc.go.tz](http://sikongedc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)  
Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge  
4 Mtaa wa Bomani  
S.L.P 70  
45382 - SIKONGE TABORA

7/06/2023

**TANGAZO LA ZABUNI YA KUMPATA MWEKEZAJI  
KATIKA KIWANDA CHA KATI CHA KUCHAKATA MAZAO  
YA NYUKI. – LGA/121/2021/2022/NC/08  
MARUDIO**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge anawatangazia Wazabuni /Makampuni / Wajasiliamali / Ushirika au Wananchi wenye uwezo wa Kuwekeza katika Kiwanda cha kati cha Kuchakata mazao ya Nyuki kilichopo katika kijiji cha Mlogolo kata ya Sikonge.

**SIFA ZA KIWANDA**

- Kiwanda kina mitambo yenye uwezo wa kuchakata tan 4 za mazao ya nyuki kwa siku.
- Kiwanda kipo karibu na barabara kuu ya lami iendayo Tabora Mjini na Mkoani Katavi.
- Kinamazingira mazuri na rafiki kwa uwekezaji.
- Kiwanda kina miundo mbinu kama maji, umeme wa kutosha kwa matumizi ya Kiwanda.
- Upatikanaji wa malighafi kwa uhakika na kwa muda wote.

## SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na leseni ya dhamana kutoka Bodi ya Usimamizi wa stakabadhi za Ghala.
- Awe na uwezo kulipia mapato (cess) ya Halmashauri.
- Awe na uwezo wa kulipa wafugaji wa nyuki baada ya kufikisha Mzigo Ghalani.
- Awe na leseni za biashara zinazoweza kuhitajika kutoka kwenye mamlaka za udhibiti.
- Awe na vibali vya Mamlaka ya Uthibiti Ubora wa viwango vinavyotambulika na Serikali

Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi ni Sikonge tarehe 20/06/2023, Jumanne saa 5.00 asubuhi katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji.

Imetolewa na;

  
Seleman M. Pandawe  
Mkurugenzi Mtendaji (W)  
**SIKONGE**